بسم الله الرحمن الرحيم

# Jibu la Swali

## Matokeo ya Kisiasa Nchini Kazakhstan

## (Imetafsiriwa)

**Swali:**

Urusi iliingilia kati kwa jina la Shirika la Mkataba wa Usalama wa Pamoja nchini Kazakhstan baada ya rais wake, Kassym-Jomart Tokayev, kuomba msaada wake katika kuzima maandamano yaliyozuka nchini mwake, baada ya bei ya gesi ya kimiminika kupanda maradufu, na kisha kupanda ghafla... Urusi ilishutumu vikosi vya nje, hasa Marekani, kuingilia masuala ya nchi na kuchochea maandamano. Pia ilitangazwa kuwa mkurugenzi wa Kamati ya Usalama wa Kitaifa ameshutumiwa kwa kupanga jaribio la mapinduzi. Nini msingi wa maandamano haya? Kwa nini Urusi iliingilia kati haraka sana kwa jina la Shirika la Mkataba wa Usalama wa Pamoja? Je, msimamo wa Marekani ni upi kuhusu hilo?

**Jibu:**

**Ili kufafanua jibu kwa maswali hapo juu, tunahakiki masuala yafuatayo:**

1- Kazakhstan, kama sehemu ya Magharibi Turkestan katika Asia ya Kati, ni nchi kubwa ya Kiislamu yenye eneo la zaidi ya milioni 2.7 km2, lakini idadi yake ni ndogo kuhusiana na eneo lake, kama wanavyokuwa na idadi ya milioni 19, wengi wao ni Waislamu, ambao asilimia yao huzidi 75%. Kuna watu wachache wa asili ya Kirusi nchini Kazakhstan, ambao wanasemekana kujumuisha asilimia 20 ya idadi ya watu, au takriban milioni 3.5. Nchi hii ni muhimu kwa Urusi kiuchumi na siasa za kijiografia, kama ilivyokuwa chini ya udhibiti wa Urusi wa moja kwa moja wakati wa Umoja wa Kisovieti, mpaka kupata uhuru wake mwaka 1991, lakini ilibakia kuhusishwa na Urusi ndani ya kile kinachojulikana kama kikundi cha majimbo ya kujitegemea, pamoja na Shirika la Mkataba wa Usalama wa Pamoja na Mkataba wa Shanghai. Kituo cha angani cha Urusi, Kazakhstan, kipo katika Baikonur Cosmodrome, ambapo makombora ya kubeba yanayobeba vyombo vya angani huzinduliwa. Urusi ilikuwa ikidhibiti utajiri wake mkubwa. Ni matajiri katika mafuta kama inavyohusisha asilimia 21 ya Pato la Taifa na hutoa mapipa zaidi ya milioni 1.5 ya mafuta kwa siku.

Ni moja ya wazalishaji wakuu wa uranium duniani. Nchi hii ya Kiislamu ina hifadhi ya uranium ya tani milioni 1.5. Ina kiasi kikubwa cha manganese, chuma, chromium, makaa ya mawe, pamoja na gesi ya asili. Hadi sasa, mita za ujazo bilioni 2 za gesi ya asili zimegunduliwa. Kwa hiyo, Kazakhstan ni muhimu kwa Urusi, kama ilivyo katika nafasi ya pili baada ya Ukraine ambapo Urusi inaliona kuwa eneo lake muhimu la ushawishi katika nafasi ya zamani ya Soviet. Kwa sababu hii, inajitahidi kila jitihada za kuendelea kuimiliki ili kile kilichotokea Ukraine, ambapo kwa kweli ilikuwa huru kutokana nayo si tu kwa jina kama Kazakhstan, halijirudii tena!

2- Amerika pia inafahamu umuhimu wa Kazakhstan, kama eneo muhimu ambalo liko kwenye mipaka ya kusini ya Urusi, na katika mipaka ya magharibi ya China, na hivyo Amerika inatamani kupanua ushawishi wake nchini humo ili kuzunguka Urusi kutoka upande huu na kuinyima ushawishi wa kikanda katika eneo hilo. Na pia kuifungia China kutoka upande mwingine. Aidha, kuondoka kwa nchi hii kutoka kwa mikono ya Urusi kunaweza kusababisha kuondoka kwa nchi zote za Asia ya Kati kutoka kwa udhibiti wa Urusi na nje ya ushawishi wake. Maslahi haya ya Marekani yameonekana tangu tamko la uhuru wa Kazakhstan, kama ilivyokuwa nchi ya kwanza kutambua uhuru wa Kazakhstan, na kisha makampuni ya Amerika yalianza kuingia Kazakhstan na kupata sekta nyingi za mafuta na gesi nchini. Kwa mfano, kampuni ya Marekani Chevron inapata 50% ya uwanja wa mafuta ya Tengiz, ambayo ni sehemu ya tatu ya pato la kila mwaka. Makampuni ya Ulaya pia yalianza kupata sehemu ya rasilimali za nishati za Kazakhstan. Inasemwa kuwa ["karibu 90% ya mauzo ya nje ya Kazakhstan ni rasilimali za nishati kama vile mafuta na gesi, karibu ambayo yote yamedhibitiwa na kumilikiwa na mabepari wakuu wa Magharibi, na makampuni makubwa ya Amerika na Ulaya." (Shirika la Sputnik la Urusi 8/1/2022)] Majaribio ya Amerika hayakuwa tu kwa makampuni ya mafuta na gesi, lakini yalikwenda zaidi ya hayo kwa kutia saini mikataba fulani ya kijeshi wakati wa utawala wa Nazarbayev, uliotawala tangu 1989 hadi alipotangaza kujiuzulu Machi 2019. Kisha wakati wa mrithi wake baada ya hapo. Lakini uhusiano wao wa karibu na Urusi ulizuia Amerika kuhitimisha makubaliano ya kijeshi yenye ufanisi. Hata hivyo, Amerika haikukata tamaa na majaribio yake; wakati wa ushuhuda wake mbele ya Seneti mnamo Februari 2019, Kamanda wa Kitengo Kikuu cha Kijeshi cha Marekani wakati huo, Generali Joseph Votel, alisema kuhusu uhusiano wa Marekani na Kazakhstan: ["Inachukuliwa kuwa uhusiano wa imara zaidi katika Asia ya Kati" akinikuu al-Jazeera 6/1/2022)]. Mawasiliano kati ya majeshi ya Marekani na Kazakhstan ni kipengele muhimu cha mahusiano kati ya nchi hizo mbili. Tangu mwaka 2003, Kazakhstan imeshiriki katika uendeshaji wa mazoezi ya kijeshi ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na zoezi moja ambalo lilifanyika kusini mashariki mwa Kazakhstan mwezi June 2019, ambapo majeshi ya Marekani yalishiriki. Ingawa ilikuwa karibu na mazoezi ya kawaida, lakini inaonyesha maslahi ya Marekani huko Kazakhstan, na Urusi bila shaka inaogopa maslahi haya.

3- Hofu ya Urusi iliongezeka wakati maandamano hayo yalipotokea na ghafla kupanuka! Matukio haya yalikurupuka, kama inavyoonekana, na maandamano dhidi ya kupanda mara mbili kwa bei ya gesi, kutoka kwa wakazi wa miji ya Zanauzin na Aktau upande wa magharibi mwa nchi 5/1/2022, lakini yalipanuka na kuenea katika miji mingine, Almaty ambao ni mji mkuu wa zamani wa nchi na mkubwa na moja ya miji muhimu ya kibiashara. Iliripotiwa kuwa maandamano hayo yalifika makaazi ya rais jijini, pamoja na jengo la manispaa. Shirika la Sputnik la Urusi lilisema kuwa "vikosi vya usalama viliweka vizuizi vya usalama karibu na jengo la utawala wa mji mkuu, Nur-Sultan (zamani Astana), na kwamba wakaazi wa mji mkuu walikimbia kutoa fedha zao kutoka kwa mabenki kwa kiasi kikubwa, katikati ya kukomeshwa malipo yasiyo ya fedha kutokana na kukatizwa kwa mtandao. "

Vyombo vya habari vya mitaani viliripoti kwamba "wafanyakazi wa madini katika mkoa wa mashariki mwa Balkhash walijiunga na maandamano na kusimamisha kufanya kazi." Kwa hiyo, maandamano yalianza kugeuka kuwa vurugu ... Balozi wa Kazakh jijini Ankara alitoa maoni juu ya matukio ya nchi yake, akisema: ["Mwanzo wa maandamano ulikuwa na lengo la kudai hali bora ya maisha na kupinga kupanda kwa bei ya gesi. Baada ya kuhamia mji wa Almaty, ilichukua njia tofauti na ikahusishwa na maneno ya uchochezi na matendo ambayo ni kinyume cha sheria. "( shirika la ADADOLU 6/1/2022)]. Kujiuzulu kwa serikali ya Kazakh kulitangazwa mnamo tarehe 5/1/2022 katika jaribio la kutuliza hali hiyo na kupunguza bei ya gesi. Lakini maandamano hayakuacha, lakini badala yake yalipanuka na kuendelea zaidi!

4- Upanuzi huu ulisababisha Urusi, kabla ya Kazakhstan, kumshtumu pande mbili:

A-sababu ya nyuma yake, ilikuwa kwamba habari iliripotiwa kuwa baadhi ya walinda usalama walikuwa wamefumbia macho maandamano na machafuko hayo, na kisha kidole cha lawama kikaelekezwa kwa Mkurugenzi wa Kamati ya Usalama wa Taifa (Huduma ya Upelelezi) Karim Masimov, ambaye ana wajibu wa kudumisha usalama nchini. Kana kwamba mtu huyu alitumia fursa hiyo kuchukua mamlaka. Kwa hiyo, alifukuzwa kazi mnamo 8/1/2022 na kushtakiwa kwa uasi. [Kamati ya Usalama wa Taifa ya Kazakhstan ilitangaza kukamatwa kwa kiongozi wake wa zamani, Karim Masimov, kwa kutuhumiwa kwa "uasi." Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Usalama wa Taifa: "Mnamo Januari 6 ya mwaka huu, Kamati ya Usalama wa Taifa ilizindua uchunguzi kwa madhumuni ya jaribio la juu la uasi, kulingana na kifungu cha 175 cha sehemu moja ya Kanuni ya Jinai ya Jamhuri ya Kazakhstan." (RT 8/1/2022), Yermukhamet Yertssayev, mshauri wa zamani wa Rais wa zamani wa Kazakhstan, Nursultan Nazarbayev, hivi karibuni alisema [kwamba moja ya sababu za mgogoro nchini ni usaliti wa viongozi wengine wakuu. Alielezea kilichotokea nchini hivi karibuni kama "jaribio la mapinduzi na uasi wa kisilaha," na kusema: "Kiwango cha jaribio hili la mapinduzi na uasi wa kisilaha kinashangaza, na ni jaribio la kupangwa na la kinguvu, ambalo haliwezekani kutekelezwa bila wasaliti katika viwango vya juu vya utawala, hasa mamlaka ya utendaji." (RT, 8/1/2022)]

B- Rais Kassem Tokayev baadaye alitangaza ombi lake la kuingilia kati Shirika la Usalama la Pamoja lililoongozwa na Urusi, akisema: ["Nchi yake ilikuwa chini ya mashambulizi ya kigaidi na kitendo kilichopangwa na cha kivamizi kwa ushiriki wa wapiganaji wa kigeni..." Aliongeza kuwa "vitendo vya unyanyasaji na kigaidi vilisababisha kuangamia kwa wahasiriwa wengi miongoni mwa wanachama wa huduma za usalama na raia. Karibu vituo vya biashara 1,300 viliharibiwa, vituo vya biashara zaidi ya 100 na mabenki vimeshambuliwa, magari 500 ya polisi yalikuwa yamechomwa moto, na hasara zilikuwa kati ya dolari bilioni 2 na 3." Aliongeza, akitangaza "kukamatwa kwa watu elfu 10, na kutangaza utulivu wa hali, na kwamba hali imedhibitiwa, vituo vya vitisho vya kigaidi vimedhibitiwa, na mitambo muhimu ya kimkakati na maeneo ya kuhifadhi silaha na risasi zimehifadhiwa." (Russia Today 10/1/2022)].

C- Kwa hiyo, Rais wa Kazakhstan Tokayev aliomba Urusi kuingilia kati, na Warusi waliitikia haraka, kana kwamba walikuwa wameamua kuingilia kati kabla ya kuombwa! Kwa hiyo, walianzisha uingiliaji wa kijeshi huko Kazakhstan kupitia shirika la pamoja la usalama, ambalo lilianzishwa mwaka 1992, na lilipeleka kikosi cha kwanza cha kijeshi mnamo 6/1/2022 ... (Al-Jazeera Net 6/1/2022). Kisha, katika siku mbili zilizofuata, wanajeshi 2500 na vifaa vyao na magari ya kijeshi yalisafirishwa kwa ndege. Ndege zaidi ya 70 za kijeshi zilishiriki katika ujumbe huu wa dharura, ikiwa ni pamoja na uhamisho wa askari kutoka Armenia na Kyrgyzstan kwenda Kazakhstan, na kwa hili Tokayev alisema: ["Ninashughulikia maneno maalum ya shukrani kwa Rais wa Urusi Putin, ambaye aliitikia kwa haraka ombi langu la msaada. " (Russia Today 7/1/2022)].

Baada ya hapo, Putin alisema katika mkutano wa video wa Halmashauri ya Usalama wa Pamoja wa Shirika la Usalama wa Pamoja mnamo 10/1/2022, akisema: ["Vikosi vingine vya nje na vya ndani vimetumia fursa ya hali ya kiuchumi huko Kazakhstan kufikia malengo yao. Shirika la makubaliano ya usalama wa pamoja liliweza kuchukua hatua muhimu ili kuzuia kuzorota kwa hali hiyo nchini Kazakhstan. Nimechukua uamuzi muhimu kwa wakati na kwamba majeshi haya yatabaki Kazakhstan kwa kipindi kitakachoamuliwa na rais wa nchi hii. Matukio Katika Kazakhstan sio ya kwanza na hayatakuwa ya mwisho kwa kuingiliwa nje. Nchi za Shirika la Mkataba wa Usalama wa Pamoja limeonyesha kuwa hawataruhusu mapinduzi ya rangi. Na matukio ya hivi karibuni nchini Kazakhstan yanathibitisha kwamba baadhi ya majeshi hayatakoma kutumia mitandao ya kijamii ili kuajiri watu wenye nguvu na magaidi na kuunda seli za wapiganaji. "(Russia Today 10/1/2022)].

Upande wa pili, unatoka nje:

Ingawa Putin hakutaja katika taarifa yake wakati wa mkutano wa shirika la usalama, kwamba Amerika haijahusika na chochote katika matukio hayo, kwa maneno yake, lakini hili linaeleweka wazi kutokana na maana. Nini kilichoripotiwa na vyombo vya habari vya Urusi kabla ya kuthibitisha ufahamu huu, walizungumza kuhusu jukumu la Marekani la kudhaniwa katika maandamano. Pia imethibitishwa na majibu ya msemaji wa White House Jen Psaki wakati akielezea kile kilichoripotiwa na vyombo vya habari vya Urusi kama ["madai ya kirongo ya Urusi" kuhusu wajibu dhanifu wa Marekani katika maandamano yaliyoikumba Kazakhstan, akisisitiza kuwa madai haya "Hayana ukweli kabisa", na kufichua "mkakati wa Urusi kutoa habari za kirongo." (Independent Arabia, 7/1/2022)]. Ili kuhalalisha uingiliaji wa Urusi kwa njia ya shirika la pamoja la usalama, mkuu wa sasa wa shirika, Waziri Mkuu wa Armenia Nikol Pashinyan, alithibitisha (kwamba umoja huo ulijibu ombi ambalo lilikuja kutokana na "kuingiliwa kutoka nje." (Independent Arabia 7/1/2022). Kwa maana nyengine, maneno haya yote yanaonyesha kwamba Kazakhstan, na Urusi ikiwa nyuma yake, bali mbele yake, inaona kwamba matukio haya si kwa sababu za kindani, lakini Amerika inahusika nayo. .. Ushiriki huu wa Marekani katika matukio haya unaonekana kutokana na mapitio ya taarifa zifuatazo za Marekani:

A-Blinken alitoa wito, wakati wa mazungumzo ya simu na mwenzake wa Kazakh, ili kupata suluhisho la amani kwa hali tete huko Kazakhstan na kuheshimu uhuru wa vyombo vya habari. Msemaji wa Idara ya Nchi ya Marekani Ned Bei alisema kuwa, "Blinken alisisitiza msaada kamili wa Marekani kwa taasisi za kikatiba za Kazakhstan na kutetea azimio la amani, haki-kuheshimu katika mgogoro huo." Alisema, "Amerika ina wasiwasi juu ya matukio ya Kazakhstan, lakini anaamini kwamba Jamhuri inaweza kukabiliana nayo bila msaada wa shirika la mkataba wa usalama wa pamoja. (AFP 6/1/2022)

B- Blinken alisema, akizungumza juu ya Rais wa Kazakh Kassym Tokayev kuhusu kuwapiga risasi waandamanaji ("Ninashutumu maneno hayo, na kama hiyo ni sera ya kitaifa, ninaishutumu." (CNN 9/1/2022). Rais wa Kazakh alitangaza, "Nilitoa amri ya kupiga magaidi bila ya onyo," aliongeza, "magaidi 20,000 walishiriki katika shambulizi la jiji la Almaty."

C- Amerika ilitaka kuondoka kwa majeshi ya Urusi kutoka Kazakhstan. Msemaji wa Wizara ya Nje ya Marekani alisema: ["Majeshi ya CSTO lazima yaondoke haraka Kazakhstan ... na uwepo wao unafufua maswali. Ni wajibu waondoke Ili kuimarisha ahadi yao ya kuondoka kwa haraka Kazakhstan." (RIA Novosti 11/1/2022)].

Kutokana na upinzani huu wote wa Amerika kupinga majeshi ya Urusi Kazakhstan, na kudai kwamba matatizo yake yanapaswa kutatuliwa bila kuingiliwa kati na Urusi, na kwamba haipaswi kutumia nguvu dhidi ya waandamanaji. Amerika inafahamu kuwa hii inaimarisha uwepo wa Urusi huko Kazakhstan na ushirika wa serikali hiyo na Urusi ... Ilikana shutma dhidi yake kuingilia kati katika matukio hayo, lakini sauti ya hotuba yake ilikuwa inataka kuwa maandamano yasisitishwe kwa nguvu na kutaka kwa haki za binadamu kuzingatiwa.

**Hitimisho:**

A- Ni wazi kutoka kiwango cha juu cha umuhimu kwamba Urusi inaunganisha Kazakhstan. Urusi imesimama nyuma ya kuamsha masharti ya mkataba wa pamoja wa usalama ili kuondokana na maandamano ya Kazakhstan kwa nguvu na moto, na hii ni mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa shirika la jina moja mwaka 1992, licha ya matukio ambayo yalikumba baadhi ya nchi zilizo chini ya mkataba bila kuingiliwa kati na shirika hilo, na hii inaonyesha kiwango cha umuhimu huo unaohusishwa na Kazakhstan.

B- Kwa upande mwingine, kukosekana kwa hali ya usalama nchini Kazakhstan kumeonyesha udhaifu mpya wa ushawishi wa Urusi katika mazingira ya mkoa huo wa Soviet, na hii inaweza kuvutia Magharibi kuizunguka Urusi na msururu wa migogoro inayotokana na Asia ya Kati hadi Belarus!

C- Hata hivyo, Amerika haikuweza kufanikisha kila kitu ilichotaka kutokana na majaribio yake ya kupanua ushawishi wake nchini Kazakhstan, na inaonekana kuwa ilikuwa imeridhika na maendeleo ya maandamano na ilitaka kuyatumia, na kuchukua fursa yake kuwa na wanaume ndani ya nchi, na kisha kuwa na uwezo wa kuweka shinikizo kutoka ndani na nje.

D- Ni jambo la kusikitisha kwamba maadui wanagombania juu ya nchi ya Kiislamu kama Kazakhstan, kupora mali yake, na kutumia nafasi yake na uwezo kwa maslahi yao. Wakati ambapo mawakala, wa watu wa nchi, wanajali tu juu ya mashindano ya viti na kupata nafasi za juu, wakiacha watu wa nchi maskini na mateso wakati nchi yao ina utajiri katika nchi yake na mafanikio yake, ingawa wengi wa watu wake ni Waislamu, na Uislamu umewaamrisha wasiwape makafiri njia ya kutawala juu yao ... Kwa hivyo, kuna umuhimu wa kufanya kazi ili kusimamisha Khilafah Rashida kwa njia ya Utume Ili kuokoa nchi na watu. Kisha Ummah huu utarudi kama ulivyokuwa Ummah bora uliotolewa kwa wanadamu, wenye nguvu na ushindi.

[وَلَيَنْصُرَنَّ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ]

**"Na bila shaka Mwenyezi Mungu atawasaidia wale wanaomsaidia Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mtukufu"** [Al-Hajj: 40]

**12 Jumada II 1443 H**
**15/01/2022 M**